

SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA



TAARIFA KWA WAZALISHAJI, WAUZAJI NA WASAMBAZAJI WA MIKATE NA MAANDAZI

Dar es salaam, Machi 13, 2020.

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) lenye dhamana ya kuwezesha biashara na kumlinda mlaji/mtumiaji, limebaini uwepo wa mwenendo usiofaa wa usafirishaji na usambazaji wa mikate na maandazi unaofanywa na baadhi ya waendesha pikipiki au baiskeli ambapo bidhaa hizo hufungwa na kuning'inizwa moja kwa moja kwenye pikipiki au baiskeli pasipo kuwekwa kwenye makasha maalum ya kubebea.

Usafirishaji wa namna hiyo ni hatarishi kwani huweza kusababisha bidhaa za mikate na maandazi kuchafuliwa na vimelea vya maradhi au kemikali za sumu na hivyo kuhatarisha usalama wa walaji.

Kwa taarifa hii, TBS inapenda kuwataarifu wazalishaji, wasambazaji na wauzaji wa bidhaa za mikate, maandazi na aina yoyote ya vitafunwa kuhakikisha kuwa bidhaa hizo zinawekwa kwenye makasha maalum ya kubebea kabla ya kuzisafirisha kwa pikipiki, baiskeli au vyombo vingine vya usafiri kwa lengo la kuhakikisha usalama na ubora wake ili kulinda afya ya walaji.

Kwa yeyote atakayekiuka agizo hili, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake. Aidha, Shirika litaendelea kuimarisha ukaguzi na ufuatiliaji ili kuhakikisha agizo hili linazingatiwa.

Imetolewa na;

Roida Andusamile
Mkuu wa kitengo cha Uhusiano

